**OFISI YA RAIS,**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA**
**UKANDA WA MAGHARIBI**
**MTIHANI WA KIDATO CHA PILI**

**021** **KISWAHILI**

**Muda : Saa 2:30** **JUNI 2022**

**MAELEKEZO**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D, na E, zenye jumla ya mawsali kumi (10)
2. Jibu maswali yote
3. Sehemu A ina jumla ya alama 15. Sehemu, B na C zina alama ishirini (20) kila moja. Sehemu D ina alama thelathini (30) na Sehemu E ina alama15.
4. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa bluu au mweusi.

**SEHEMU A( ALAMA 15)**

**UFAHAMU**

Soma wimbo ufuatao, kisha jibu maswali yafuatayo;-

Jamani! Jamani! Vijana mko wapi? Mabinti mko wapi! Ninatamani kusoma lakini mambo yamekuwa mengi! Ndi! Ndi! Ndi! Shule naipenda lakini mambo ni mengi! Ndi! Ndi! Nifanyaje jamani mie………………. Ili na mimi nifaulu kama wengine,……..

Siku hizi mambo yamebedilika, kusoma, kuandika muhimu Sayansi na Teknolojia inajionesha waziwazi mambo yamekuwa mengi ……. Ndi! Ndi! Ndi! Nifanyaje jamani mie ili na mimi nifaulu kama wengine.

MASWALI

1. a) Taja kichwa cha wimbo uliosoma ……………………………………………………
   .........................................................................................................................
   b) Mwimbaji yupo katika hali gani?……………………………………………………
   …………………………………………………………………………………....
   c) Jitihada gani azifuate ili apate elimu…………………………………………………
   …………………………………………………………………………………..
   d) Fafanua ujumbe wa mwimbaji katika wimbo huu……………………………………………
   ………………………………………………………………………………………
   e) Taja kibwagizo cha wimbo uliosoma…………………………………………………..
   ………………………………………………………………………………………
2. Fupisha wimbo uliosoma kwa maneno kati ya ishirini na tano (25) na thelathini (30).

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………...................

**SEHEMU B: (ALAMA 20)**

**3. a**) Bainisha mzizi wa asili wa kila kitenzi katika sentensi zifuatazo:

(i) Watoto walifungiana milango……………………………………
(ii) Sisi hatupendani ……………………………………………
(iii) Jana hatukusomeana …………………………………………
(iv)Mvua ilinyesha leo asubuhi ..........................................................
(v) Juma anaruka kamba .........................................................................

(b) Oanisha **orodha A** na **orodha B** ili kujenga dhana sahihi. Onesha majibu yako eneo liliwekwa kujibia

| **Orodha A** | **Orodha B** |
|---|---|
| i. Wamewaibia<br>ii. Zawadi <u>*za mtwara*</u> tamu sana<br>iii. <u>*U*</u> mtoto wa mzee Mkanyageni<br>iv. Jioshe<br>v. Mnyumbuliko<br>vi. Joto laweza kusafiri kwa njia ya mnunurisho<br>vii. Neno lenye fonimu 3<br>viii. Mofu<br>ix. Foni<br>x. Oa | a) Uambishaji wa maneno<br>b) Kivumishi cha a-unganifu<br>c) Kiwakilishi<br>d) Kitenzi kishirikishi<br>e) Oneshea<br>f) Kiambishi cha nafsi ya pili wingi<br>g) Agizo<br>h) Kitenzi<br>i) Mnyumbuliko wa kitenzi<br>j) Chai<br>k) Umbo linalodhihirisha vitamkwa<br>l) Ni sauti za lugha<br>m) Mbao<br>n) Kosa la kimsamiati<br>o) Shina la silabi 2<br>p) Ni maumbo ya lugha<br>q) Kosa la mpangilio wa sauti<br>r) Shina la silabi moja<br>s) Umbo linalodhihirisha mofimu |

**4)** Bainisha dhima za mofimu zilizopigiwa mstari katika maneno yafuatayo:

i) <u>Si</u>taki…………………………………..…………………

ii) A<u>me</u>kichukua………………..………………………

iii) Wali<u>ji</u>ua………………………………………………

iv) Hawa<u>ku</u>soma…………………………………………

v) Ame<u>ku</u>piga……………………………………………

**5 a)** Bainisha aina za maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo:
i) Viti <u>vizuri</u> vimepangwa vizuri
ii) Wale wawili wa Mwanza <u>ni</u> ndugu zetu
iii) <u>Kucheza</u> kwake kuna faida
iv) Alifika <u>ingawa</u> alikuwa na taarifa
v) <u>Ah!</u> Mwenzetu ameumia

**b)** Kwa kuzingatia matmizi ya kamusi, panga majina yafuatayo kwa mpangilio sahihi

i) John ii) Johari iii) Jobson iv) Jonas v) Johnson

## SEHEMU C: (ALAMA 20)
## MAWASILIANO NA UTUMIZI WA LUGHA

**6.** a) Fafanua istilahi zifuatazo:
i) Lafudhi ii) Utata katika tungo iii) Shina iv) Mzizi v) Simo

**7. a)** Taja dhima tano za rejesta

b) Toa tofauti tano (5) kati ya lugha ya mazungumzo na lugha ya maandishi

**c)** Chagua jibu sahihi kisha jibu nafasi zilizoachwa wazi kwa kuandika herufi ya jibu sahihi

i. ...................................... ni kitendo cha kupashana habari au taarifa baina ya watu wawili au zaidi.
a) Lugha
b) Mawasiliano
c) Kiswahili
d) Kuwasiliana
ii. .................... ni silabi au mkusanyiko wa silabi zinazobeba maana.
a) Sauti
b) Silabi
c) Sentensi
d) Neno
iii. Ipi siyo dhima ya lugha..........................................................
a) Hutenga baadhi ya watu
b) Huelimisha
c) Utambulisho wa jamii
d) Ni sehemu ya utamaduni
iv. .........................ni utaratibu wa kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti
a) Kiimbo
b) Mkazo
c) Neno
d) Sentensi
v. .........................................muunganiko wa maneno
a) Tungo neno
b) Aya
c) Sentensi
d) Sauti

## SEHEMU D: (ALAMA 30)

## FASIHI KWA UJUMLA

**8**. **a]** Fafanua istilahi zifuatazo za kifasihi

i] Maigizo…………………………………………………………………………
ii] kituo bahari………………………………………………………………………………..
iii] Tarihi……………………………………………………………………………..
iv] Majigambo………………………………………………………………………..
v] Mizani…………………………………………………………………………………..

**b)** Kamilisha methali zifuatazo
i) Kibuzi na kibuzi…………………………..
ii) ………………………………mwisho wa uhunzi
iii) Kipya kinyemi……………………………………..
iv) Haram yako……………………………….
v) Nia njema tabibu, nia mbaya………………………..

**(c)** Toa maana za nahau zifuatazo;
i. Kumezea mate.................................................
ii. Kuwa na mate ya fisi........................................................
iii. Mwenye ndimi mbili............................................
iv. Mbiu ya mgambo .......................................................
v. Mtu mwenye mkono wa birika ....................................................

**(d)** "Semi ni moja ya tanzu nne zinazounda fasihi simulizi." Thibitisha kauli hii kwa kubainisha Vipera vitano (5) vya semi.
i)…………………. ii)………………… (iii)……………....(iv)………………(v)……………..…

**9.** Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata

Si leo toka zamani, mkulima mtu duni
Ana tabu maishani, tena hana thamani
Yafaa tutizameni, tena tuyachunguzeni
Si leo toka zamani, mkulima mtu duni

Jogoo linapowika, kokoriko mitaani
Mkulima huamka, jembe lake mkononi
Bila ya kupumzika, hufika kwake shambani
Si leo toka zamani, mkulima mtu duni

Maswali:
i) Kichwa cha shairi hili ni ………………….
ii) Kila mshororo wa kila beti una mizani ngapi?
iii) Kina cha kati cha ubeti wa kwanza ni…………..na cha mwisho ni………………
iv) Kituo cha shairi hili ni kipi?...........................
v) Shairi hili lipo katika kundi gani la shairi?........................

## SEHEMU E: (ALAMA 15)
## UANDISHI

**10.** Wewe unaitwa Jofrey Sanga Afisa rasilimali watu, unafanya kazi kwenye kampuni ya baba yako ya uzalisha wa viatilifu S.L.P 502 Mwanza na baba yako ndiye mkurugenzi wa kampuni hiyo. Mwandikie barua baba yako ukiomba kwenda kumwangalia bibi yako ambaye anaumwa.